# Twende Pamoja

HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

Hutolewa kila baada ya miezi Mitatu Octoba-Disemba 2016 Toleo Na 006



Ndani



Shule za Sekondari Halmashauri ya Wilaya zapewa vitabu vya Sayansi Uk........8

Mnada wa Ilunda Mkombozi wa wakulima na wafugaji Njombe Uk...........6



Habari katika picha Uk.11&12


# Madiwani wapitisha bajeti ya Bilioni 21 kwa shughuli za Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2017/2018



*Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe Valentino Hongoli akifungua kikao maalumu cha baraza la madiwani kwa ajili ya kupitia mapendekezo ya mpango wa bajeti kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2019*

## Milioni 300 kujenga mradi wa Umwagiliaji kijiji cha Itipingi Njombe.



*Utiaji saini mkataba wa mradi wa umwagiliaji Kijiji cha Itipingi wenye thamani ya zaidi ya Tsh 300 Milioni unatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe*

## Watoto chini ya umri wa miaka mitano 12,855 wasajiliwa Halmashauri ya Wilaya Njombe





*Kushoto ni baadhi ya wananchi wa kijiji cha Ikondo na kulia ni wananchi wa Kijiji cha Itunduma wakiwa katika mistari kwa ajili ya kuandikisha watoto chini ya umri wa miaka mitano.Habari Kamili ukurasa wa 5*

# Tahariri

Moja ya jukumu la Halmashauri ni kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato kulingana na eneo husika Halmashauri ilipo. Mapato yanayopatikana yamekuwa yakitumika katika shughuli mbalimbali ikiwemo kutekeleza miradi ya maendeleo, kununua dawa katika vituo vya afya na zahanati n.k

Bila kukusanya mapato Halmashauri haiwezi kujiendesha na tayari waziri Mkuu Kassim Majaliwa alishatangaza kuwa Halmashauri itakayoshindwa kukusanya mapato kwa asilimia 80 basi itafutwa.

Tunaliongea hili kwa sababu kumekuwa na baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali kukwepa kulipa ushuru ambao uko kwa mujibu wa sheria na wakati mwingine wamekuwa ni wasumbufu.

Kupitia safu hii Halmashauri inawataka wafanyabiashara kuacha mara moja tabia hiyo ikiwemo kusafirisha mazao ya misitu usiku jambo ambalo ni kosa kisheria kwa mujibu wa tangazo la serikali namba 369 (1999), ambapo mtu anayetenda kosa hilo atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwemo kufungwa jela miezi 6 au kutozwa faini ya shilingi 300,000 Serikali Kuu kwa kusafirisha mazao hayo usiku, Pamoja na faini ya kati ya shilingi 50,000 hadi 300,000 kwa Halmashauri.

Ili kuepukana na usumbufu usiokuwa wa lazima Halmashauri inapenda kuwashauri wafanya biashara na wamiliki wa vyombo kulipa ushuru kulingana na idadi ya mzigo husika.

Moja ya hasara kubwa wanayoipata wafanyabiashara ni kulipa faini pamoja na kupoteza muda mwingi barabarani.

Unakuta mfanya biashara analipa faini kiasi cha shilingi 300,000 kwa kufanya udanganyifu wa kutolipia mbao ambazo gharama yake ni Tsh 40,000/.

Pamoja na kulipa faini mmiliki wa chombo cha usafiri anapata hasara sababu muda ambao anatumia kusubiri mfanyabiashara atafute pesa ili aweze kulipia ungemwezesha kufika sehemu ambao alitakiwa kupeleka mzigo na kupata mteja mwingine lakini anatumia kusubiri maana mara nyingine gari hushikiliwa kwa zaidi ya masaa 6.

Halmashauri inatoa wito kwa jamii, wamiliki wa vyombo vya usafiri pamoja na wafanya biashara kujiepusha na vitendo vya udanganyifu kwa kuwa Halmashauri imejipanga kikamilifu kuhakikisha mianya yote ya utoroshaji wa mbao na vyanzo vingine vya mapato inadhibitiwa.

"Twende Pamoja"

Linatolewa na Ofisi ya

Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya

Njombe.

S.L.P 547 Njombe.

Phone: 026 2782111

Fax: 026 2782857

Email:ded@njombedc.go.tz

info@njombedc.go.tz

njombedc@yahoo.com

Tovuti:www.njombedc.go.tz

BODI YA UHARIRI.

MONICA PZ KWILUHYA- MKURUGENZI MTENDAJI
LUKELO MSHAURA- MHARIRI MKUU
CHRISTOPHER HAULE -MHARIRI
ABRAHAMU KAAYA-MHARIRI.

## SERA YA UHARIRI.

Madhumuni ya Jarida hili ni kuhabarisha na kuelimisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya wilaya ya Njombe. Aidha Sera , mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inafafanuliwa kupitia Jarida hili . Isipokuwa pale itakapokatazwa habari za Jarida la Twende Pamoja zinaweza kunukuliwa mradi Mhariri ajulishwe kwa maandishi.

# Madiwani wapitisha bilioni 21 kwa shughuli za Halmashauri mwaka wa fedha 2017/2018

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Njombe, Mkoani Njombe limepitisha mapendekezo ya rasimu ya mapendekezo ya bajeti kwa ajili ya mwaka wa fedha 2017/2018 kwa Halmashauri hiyo.

Katika mapendekezo hayo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inatarajia kukusanya na kutumia kiasi cha shilingi 21.821 bilioni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi, Matumizi mengineyo na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Akisoma mapendekezo hayo kwa niaba ya Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe Bi Monika Kwiluhya katika kikao maalumu cha kujadili bajeti ya Halmashauri hiyo , kaimu Afisa Mipango wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe , Steward Vidoga alisema jumla ya shilingi bilioni 5.903 zimeelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema kuwa bajeti ya mwaka 2017/2018 imeandaliwa kwa kuzingatia utekelezaji wa malengo makubwa na dira ya maendeleo ya Taifa, mpango wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano (2016/2017 -2020/2021), Mipango shirikishi ya jamii kwa kutumia fursa na vikwazo vya maendeleo iliyoibuliwa na kata 12 zilizopo katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Aliongeza kuwa bajeti hiyo imezingatia mpango mkakati wa miaka mitano wa Halmashauri, hotuba ya Rais wa Jamuhuri ya muungano wa Tanzania, John Pombe Magufuli aliyoitoa wakati akizindua bunge la 11pamoja na maelekezo yaliyotolewa katika ilani ya chama cha mapinduzi kwa mwaka ya mwaka 2015.

Katika kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezeka Halmashauri ya wilaya ya njombe imebuni vyanzo vipya vya mapato ikiwemo kuanzishwa kwa mnada wa mifugo kijiji cha Ilunda, kuanzishwa kwa soko la mbao kijiji cha matembwe pamoja na kuandika maandiko ya miradi kwa ajili ya kufanya uwekezaji mkubwa katika eneo la Halmashauri lililopo Njombe mjini lenye zaidi hekari nne ambapo Halmashauri inatarajia kupata mwekezaji atakayejenga ofisi, kumbi za mikutano pamoja na maduka ya kisasa.



*Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wakifuatilia mjadala wa mapendekezo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya Njombe.*

Bajeti ya Halmashauri ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa mwaka 2016/2017 ilikuwa ni kiasi cha 21.385 ambapo hadi sasa utekelezaji wake unaendelea.

Bw Vidoga alivitaja vyanzo vya mapato kuwa ni fedha kutoka Serikali kuu, michango ya jamii, wafadhili pamoja na Halmashauri ya Wilaya kupitia mapato ya ndani.

Akichangia mapendekezo ya bajeti mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe , Valentino Hongoli, aliwataka viongozi wa Kisiasa katika ngazi zote wajitolee kwa dhati kufanya kazi na Wataalamu wa Halmashauri katika ngazi zote katika kuhamasisha jamii ili iweze kuchangia rasilimali fedha na nguvu kazi pamoja na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyopangwa katika maeneo yao badala ya kuiachia serikali peke yake.

Kiutawala Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imegawanyika katika Tarafa 2 ambazo ni tarafa ya Lupembe na Tarafa ya Makambako huku ikiwa na Kata 12, Vijiji 45, na Vitongoji 227

# Mradi wa umwagiliaji wa Milioni 300 kujengwa kijiji cha Itipingi Njombe.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imesaini mkataba wenye thamani ya zaidi milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa mradi mkubwa wa umwagiliaji katika kijiji cha Itipingi kilichopo Kata ya Igongolo Wilayani Njombe,

Mradi huo unafadhiliwa na Shirika la JAICA kutoka nchini Japani ambao utekelezaji wake unaanza januari mwaka huu, utajengwa na mkandalasi Engineering Plus kutoka Dar es Salaama na utatekelezwa kwa kipindi cha miezi nane huku ukisimamiwa kwa pamoja baina ya wataalamu wa umwagiliaji kutoka kanda ya Mbeya na Halmashauri ya Njombe.

Akizungumza wakati wa utiaji saini wa mkataba huo uliohudhuriwa na meneja uendeshaji wa kampuni ya Engineering Plus, wawakilishi wa kikundi cha umwagiliaji skimu ya Itipingi, wataalamu kutoka ofisi ya mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe , Bi Monica PZ Kwiluhya, amewataka wakandalasi kutekeleza mradi huu kwa wakati na ubora unakubalika.

"Kawaida mimi huwa siongezi muda wa kutekeleza mradi kwa kuwa pesa tayari ipo hivyo hakuna visingizio, siko tayari kuona mradi unacheleweshwa pasipokuwa na sababu za msingi maana pesa hizi ni za wafadhili na mradi ukicheleweshwa zinatakiwa zirudi" alisema Kwiluhya.

Amewataka wakandalasi kushirikiana na wananchi kwa kazi zile ambazo zinaweza kufanywa na wananchi pamoja na kujiepusha na vitendo vitakavyopelekea kukosa ushirikiano kutoka kwa wananchi ambao ndio wamiliki wa mradi..

Kwa upande wake mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe Bw. Valentino Hongoli amewataka wakandalasi kufanya kazi kwa mujibu wa makubaliano yaMkataba kwa kuzingatia tarehe ya kuanza utekelezaji na tarehe ya kumaliza.

"Naomba mfanye kazi kwa kuzingatia thamani ya fedha na kwa viwango vinavyokubalika ili kuweza kutoa mtokeo chanya kwa wananchi" alisema Hongoli.

Kusainiwa kwa mkataba huu kunatoa matumaini kwa wananchi wa Itipingi ambapo awali walikuwa wakitumia mifereji katika kufanya kilimo cha uzalishaji wa mazao mbalimbali ikiwemo chakula na mboga mboga.

Mradi ukikamilika unatarajia kuwanufaisha zaidi ya wakazi 1500 ambao watakuwa wakilima mazao ikiwemo, mahindi, nyanya, vitunguu pamoja na mboga mboga.

Mradi huu umekuja wakati muafaka ambapo Halmashauri iko katika hatua za mwisho kukamilisha kituo cha kuzuia upotevu wa mazao ya mboga mboga na matunda ili kuyaongeza thamani ambacho kimejengwa kwa ufadhili wa shirika la MIVARAF mjini Njombe.

Sambamba na hilo mradi huu ukikamilika utasaidia kuinua kipato cha wakulima, kuongeza lishe kwa jamii pamoja na kuiongezea Halmashauri Mapato.





*Mwenyekiti wa halmashauri akiwa pamoja na wataalamu wa Halmashauri, Mkandalasi pamoja na wawakilishi wa wananchi wa kijiji cha Itipingi wakati wa utiaji saini wa mkataba wa skimu ya umwagiliaji kijiji cha Itipingi kwenye Ofisi ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.*

# Watoto chini ya miaka mitano 12,855 wasajiliwa Njombe.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imefanikiwa kuwasajili na kuwapa vyeti vya kuzaliwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano 12,855 Kupitia kampeni ya usajili wa watoto chini ya miaka mitano iliyofanyika wilayani hapa.

Kusajiliwa kwa watoto watoto 12,855 kati ya watoto 12,746 wenye umri chini ya miaka mitano sawa na asilimia 100.9 ya lengo la kusajili watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano na hivyo Halmashauri kuvuka lengo.

Usajili huo umefanyika kupitia kampeni ya kusajili watoto chini ya umri wa miaka mitano iliyofanyika katika Mkoa wa Njombe kwa kipindi cha siku 14 kuanzia Sepember 22, hadi Octaba 5 mwaka 2016 kwa ufadhili wa shirika la UNICEF kwa kushirikiana na RITA ambapo jumla ya vituo 39 vilitumika kwa ajili ya usajili wa watoto hao.

Kati ya vituo 39 vilivyokuwepo vituo 12 vilikuwa ofisi za watendaji wa Kata na vituo 27 vilikuwa ni vituo vya kutolea huduma za afya ikiwemo zahanati na vituo vya afya.

Mafanikio ya kuvuka lengo la usajili mbali na mbinu zilizotumika yanatokana na ushirikiano uliokuwepo baina ya viongozi mbalimbali kuanzia ngazi ya taifa hadi kijiji.

Katika kuhakikisha watoto wote wenye umri wa chini ya miaka mitano wanasajiliwa Halmashauri ilifanya uhamasishaji kuhusu mpango wa usajili wa watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Katika kufikisha ujumbe kwa wananchi Halmashauri ilitumia mbinu mbalimbali ikiwemo kupita katika kila kitongoji na gari la matangazo kuhamasisha, kusambaza vipeperushi, Kupeleka matangazo katika nyumba za ibada ambapo waumini walisomewa matangazo kuhusu mpango huu, kutumia vyombo vya habari hususani vile vinavyopatikana katika Wilaya ya Njombe pamoja na ngoma na mikutano ya vijiji.

Sambamba na mafanikio hayo changamoto mbalimbali zilijitokeza wakati wa utekelezaji wa kampeni hii ikiwemo tatizo la mtandao kwa kuwa usajili huu ulikuwa unafanyika kwa njia ya mtandao pamoja na baadhi ya maeneo kutofikika kwa ulahisi.

Katika kuhakikisha lengo la kampeni linafanikiwa na hakuna mtoto ambaye yuko chini ya umri wa miaka mitano anaachwa Halmashauri ilitumia mbinu mbalimbali ikiwemo kuwafuata wananchi katika maeneo yao pamoja na kufanya uandikishaji wakati wa mchana na usiku wasajili wasaidizi kuhamia maeneo yenye mtandao kwa ajili ya kuingiza taarifa.

Halmashauri inaendelea kusajili watoto wote wanaozaliwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ikiwemo zahanati na vituo vya afya.

Cheti cha kuzaliwa kinafaida kubwa kwa mtoto na utambulisho wa kwanza wa mtoto huku kikimuwezesha kupata elimu na maisha bora.

Aidha, Halmashauri inatarajia kuzitumia takwimu za usajili wa watoto katika mipango yake ikiwemo elimu na afya. Upande wa elimu takwimu hizi zitasaidia kwenye uandikishaji wa watoto wa elimu ya awali pamoja darasa la kwanza huku kwenye huduma za afya takwimu zitasaidia sana katika uagizaji wa dawa na vifaa tiba hali itakayopeleka huduma za afya kutolewa kwa ubora na kulingana na mahitaji halisi ya Halmashauri.



*Mkuu wa wilaya ya Njombe Bi Luth Msafiri akizungumza na baadhi ya wanawake wakati wa kampeni ya usajili watoto chini ya umri wa miaka mitano katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe*

# Mnada wa Wanyama waanzishwa Kijiji cha Ilunda Mtwango.

Katika kuhakikisha wakulima na wafugaji wanakuwa na soko la uhakika la kuuza bidhaa na mifugo yao Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imeanzisha mnada wa mifugo katika Kijiji cha Ilunda Kilichopo katika kata ya Mtwango wilayani Hapa.

Kuanzishwa kwa mnada huu ambao utakuwa ukifanyika kila tarehe 12 ya kila mwezi kutawawezesha wafugaji kuuza mifugo yao pamoja na wanunuzi kupata sehemu ya uhakika ya kununua mifugo kwa ajili ya ufugaji na lishe.

Mnada huu ni moja ya mikakati ya Halmashauri ya kuwainua wananchi wake kiuchumi kwa kuwawekea mazingira bora ya kuuza na kununua bidhaa mbalimbali.

Toka kuanzishwa kwa mnada huu mwitikio umekuwa mzuri ambapo wananchi mbalimbali wamekuwa wakiuza bidhaa ikiwemo mbogamboga na matunda huku kivutio kikubwa kikiwa ni nyama ya mbuzi ambayo imekuwa ikichomwa kwa ustadi wa hali ya juu na watu wa jamii ya wamasai kutoka Mbalili Mkoani Mbeya ambapo kila siku ya mnada huwa wanashiriki.

Upande wa mifugo ambayo imekuwa ikiletwa kwa ajili ya kuuzwa ni ng’ombe, mbuzi pamoja na kuku.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imeweka mikakati madhubuti katika kuboresha mnada huo na kuufanya kuwa mnada mkubwa katika mkoa wa Njombe. Tayari Halmashauri imeshaboresha vitu vya muhimu ikiwemo miundombinu ya choo na maji ya uhakika.

Halmashauri ya wilaya ya Njombe inatoa wito kwa wananchi wote kutembelea katika mnada wa Ilunda ili kuweza kujipatia kitoweo pamoja na kujifunza mambo mbalimbali kutoka kwa wakulima na wafugaji kutoka sehemu mbalimbali za mkoa wa Njombe, Mbeya na Iringa.

Aidha wakulima na wafugaji wanashauriwa kupeleka mifugo na bidhaa zao katika mnada wa Ilunda kila tarehe 12 ya kila mwezi kwa kuwa ni sehemu ya uhakika ya kuuza mifugo na bidhaa zao.

## IJUE HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe hadi sasa ina jumla ya miradi 65 ya maji inayotumia teknolojia mbalimbali katika kutoa huduma ya maji safi na salama. Miradi inayotumia teknolojia ya maji mtiririko ipo (11), inayotumia mashine ya dizeli ipo minne (4), inayotumia nishati ya umeme ipo minne (4). Miradi mingine saba (7) inatumia Hydram (Hydaulic ram) inayosukumwa na nguvu ya maji, miradi mitatu (3) inatumia pia nguvu ya maji kwa kutumia magurudumu ya yajulikanayo kama Water Wheel, Mradi wa nishati ya jua (solar) upo 1, Pia Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina visima vifupi 35 na Visima virefu (2). Kutokana na uwepo wa miradi hii, jumla ya watu 47,035 kati ya watu 85,747 sawa na asilimia 54.9% ya wananchi waliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kupata huduma ya maji safi na salama.



*Moja ya tanki la kuhifadhia maji katika kijiji cha Ukalawa Wilayani Njombe .Uwepo wa miundombinu hii unawahakikishia wananchi maji safi na salama.*

# Mradi wa umeme kilowati 430 wazinduliwa Njombe

Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Dk Medard Kalemani amezindua mradi wa umeme wa kilowati 430 unaotokana na maporomoko ya maji katika Kata ya Ikondo iliyoko Halmashauri ya wilaya ya Njombe mkoani Njombe.

Mradi huo wa umeme uliopo katika kijiji cha Ikondo umetekelezwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya CEFA kutoka Italia na kugharamiwa kwa pamoja kati yaUmoja wa Ulaya (EU) na Serikali ya Tanzania kwa jumla ya dola za Marekani 110,209 ambazo ni zaidi ya shilingi bilioni 230 za Tanzania.

Uzinduzi huo uliodhuliwa na viongozi mbalimbali ikiwemo barozi wa Tanzania nchini Tanzania, mwakilishi wa umoja wa nchi za Ulaya , Mkuu wa Mkoa wa Njombe pamoja na viongozi mbalimbali kutoka sehemu mbalimbali.

Toka kuanzishwa kwake hadi kuzinduliwa kwa mradi wa umeme kijiji cha Ikondo zaidi ya wateja 1,140 wameunganishwa na umeme katika maeneo mbalimbali ambapo mradi huu umepita kwenye Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Akizungumza wakati wa kuzindua mradi huo Dk Kalemani alisema kuwa mradi huo umetekelezwa na taasisi na utasambazwa katika vijiji vilivyoko kata za Ikondo, Matembwe na Lupembe na ziada itakayobaki itaingizwa kwenye Gridi ya Taifa.

"Habari njema ni kuwa tayari vijiji saba vimeunganishiwa umeme kupitia mradi huu, hii inatimiza moja ya malengo ya Serikali ya kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji wa nishati bora katika maeneo ya vijijini kupitia asasi za kiraia," alisema Dk Kalemani.

Alisema kuwa serikali inafanya kazi kwa bidii ili kuweza kufanikisha lengo la kuunganisha umeme kwa asilimia 75 ya wananchi ifikapo mwaka 2025.



*Naibu waziri wa nishati na madini Dr Medard Kalemani wa nne kutoka kushoto akiwa na wageni wakati wa uzinduzi wa mradi wa umeme Kijiji cha Ikondo katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.*

Awali Meneja Mradi kutoka CEFA, Jacopo Pendezza alisema taasisi hiyo ipo nchini tangu mwaka 1976 na imejikita katika miradi ya umeme vijijini na ina miradi mbalimbali ya umeme inayofanya kazi katika kata ya Matembwe, Boma la Ng'ombe na Ikondo mkoani Njombe.

Alisema kuwa awali mradi huo wa umeme wa Ikondo ulikuwa unazalisha kilowati 80 za umeme lakini kutokana na mahitaji ya wananchi kuongezeka, CEFA kwa kushirikiana na kampuni ya kijiji cha Matembwe (MVP) inayosimamia mradi huo, waliamua kuongeza mtambo wa kilowati 350 na hivyo kupelekea mradi huo kuzalisha jumla ya kilowati 430 za umeme.

Mwakilishi wa Umoja wa Ulaya katika uzinduzi huo, Jenny Nunes alisema mradi huo utakuwa na manufaa mbalimbali ikiwemo kuboresha maisha ya wananchi kiuchumi, kusaidia wanafunzi katika masomo na huduma nyingine muhimu za kijamii, na kusaidia juhudi za kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.

Aliongeza kuwa umoja huo utaendelea kusaidia miradi ya umeme nchini ili wananchi wengi wapate nishati hiyo muhimu kwa maendeleo ya uchumi.

Upande wake Mkuu wa Mkoa wa Njombe Dr. Rehema Nchimbi alieleza kuwa makao makuu yote ya wilaya za Mkoa wa Njombe yameunganishwa na umeme na huduma ya umeme inapatikana katika vijiji 250 kati ya vijiji 384 vilivyoko katika mkoa wa Njombe.

Uk 8

Inatoka Uk 7

## Mradi wa umeme kilowati 430 wazinduliwa Njombe

Wakisoma risala kwa mgeni rasmi wananchi wa Kijiji cha Ikondo walieleza kuwa wanatambua ili mradi uendelee lazima maji yawepo na kuahidi kuutunza mradi huu ikiwemo kulinda na kutunza vyanzo vya maji ili mradi uwe endelevu kwa manufaa ya kijiji chao na vijiji vingine.

Waliongeza kuwa mradi huu utaimalisha sekta ya afya , elimu pamoja na kuongeza kipato kupitia utengenezaji wa thamani na usindikaji wa mazao na kuyatafutia soka katika maeneo yenye miradi mikubwa ya Mchuchuma na Linganga mkoani Njombe.

## Shule za Sekondari zanufaika na vitabu vya masomo ya Sayansi.

Naibu waziri Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa ambaye ni mbunge wa viti maalumu mkoa wa Njombe Dr Suzan Kolimba amefanya ziara katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe na kutoa vitabu vya sayansi kwa shule za sekondari wilayani hapa.

Shule zilizonufaika na vitabu hivyo ni Sekondari ya Lupembe na Ikuna ambapo kila shule imepewa vitabu 120 na kufanya idadi ya vitabu vilivyotolewa kuwa 240. Vitabu vilivyotolewa ambavyo ni vya kujifunzia (text book) ni vya masomo ya hesabu, fizikia, kemia na baiolojia.

Akizungumza wakati wa utoaji wa vitabu hivyo Dr Kolimba alisema atahakikisha anasaidiana na wadau wengine kutatua changamoto mbalimbali ikiwemo sekta ya elimu na afya hususani vifaa tiba kwenye zahanati na hospitali.

Aliwataka wanafunzi kuvitumia vitabu walivyopewa kuongeza weredi na kuvitunza ili viweze kudumu na kutumiwa na wanafunzi wengine kwa muda mrefu. Aliwataka wananfunzi kujenga tabia ya kupenda kujisomea kwa ajili ya maendeleo ya Lupembe na taifa kwa ujumla.

Aidha, akiwa shuleni Lupembe aliahidi kuchangia mifuko 100 ya cementi kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa miundombinu katika shule hiyo.

Katika kata ya Lupembe mbali na kutembelea shule ya sekondari, alitembelea kituo cha afya Lupembe na kuangalia ujenzi wa chumba cha upasuaji unavyoendelea ambapo aliahidi kutoa mifuko 50 ya saruji kuchangia ujenzi wa miundombinu katika kituo hicho.

Akiwa katika kata ya Ikuna naibu waziri Kolimba mbali na kutoa vitabu 120 vya sayansi pia aliahidi kuchangia ujenzi wa bweni la wavulana kwa kutoa mifuko 100 ya sementi katika shule hiyo.

Wanafunzi wa shule za Lupembe na Ikuna wametoa shukrani zao kwa kupata vitabu ambavyo vitawasaidia kujifunza na kumuhakikishia kuwa watafanya vizuri katika mitihani yao.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa vitabu diwani wa Kata ya Ikuna ambaye pia ni mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe, Vallentino Hongoli, alimshukuru naibu waziri na kumtaka kuendelea na moyo huwa wa kusaidia katika Nyanja mbalimbali na kuahidi kuma ushirikiano mzuri katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kuwaletea wananchi maendeleo.



*Naibu waziri Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki Kikanda na Kimataifa (MB) Dr Suzan Kolimba (mwenye kitambaa kichwani) akikabidhi vitabu vya sayansi Shule ya Sekondari Ikuna.*

# Zaidi ya milioni 440 zatumika kuendesha Sekta ya Elimu Njombe.

Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Pombe Magufuri imetekeleza kwa vitendo ahadi ya kutoa elimu bure kwa elimu ya msingi na Sekondari baada ya kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Njombe zaidi ya Tsh 400 milioni kwa ajili ya kuendesha shule za msingi na sekondari wilayani hapa.

Fedha hizo ambazo zimetumika kuendeshea shughuli mbalimbali katika shule 10 za Sekondari na shule 52 za msingi zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ni za kipindi cha miezi 12 kuanzia mwezi Desember 2015 hadi Desemba 2016.

Shughuli zilizofanyika ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ukarabati wa miundombinu ya shule ikiwemo majengo, mifumo ya maji, umeme na samani.

Matumizi mengine ni pamoja na uendeshaji wa mitihani endelezi, uendeshaji wa michezo pamoja na kazi za utawala.

Upande wa elimu ya sekondari hadi kufikia desemba 2016 serikali ilituma Tsh 295 milioni kwa ajili ya kutumika kwenye shule 10 za serikali za sekondari zilizopo katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Aidha, shule za msingi kwa kipindi cha mwezi Desemba 2015 hadi desemba 2016 serikali imetuma Tsh. 146 milioni kwa ajili ya kutumika kwenye shule 52 za msingi za serikali zilizoko katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.

Halmashauri imeenelea kuwakumbusha wakuu wa shule kuhakikisha kuwa fedha zote zinazotumwa na serikali



*Mkaguzi wa ndani wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe Bw. Vitus Ndunguru akitoa mafunzo kwa walimu Wakuu juu ya matumizi ya fedha za elimumsingi bure*

zinatumika kwa mujibu wa miongozo iliyopo ili kuweza kuboresha kiwango cha elimu wilayani hapa.

Sambamba na hilo Halmashauri imetoa mafunzo katika Nyanja za manunuzi, uhifadhi wa vifaa vya kielimu vinavyonunuliwa pamaoja na ukaguzi.

Pamoja na nia nzuri na thabiti ya serikali ya kuhakikisha uwepo wa fursa ya elimu bora kwa wote na kuwapunguzia mzigo wazazi,walezi kugharamia na kuchangia elimumsingi katika shule za serikali lakini bado wajibu wa mzazi umebaki palepale.

Wajibu huo ni pamoja na kuhakikisha wanafunzi wanakuwa na sare za shule na michezo, vifaa vya kujifunzia vikiwemo daftari na kalamu, chakula kwa wanafunzi wa kutwa, matibabu, nauli ya kwenda na kurudi kwa wanaotumia usafiri na walioko shule za sekondari za bweni wakati wa likizo pamoja na mahitaji mengine ya kibinadamu kwa wasichana na wavulana kama vile magodoro, shuka na mito.



*Jengo la maabara katika shule ya Sekondari Lupembe wilayani Njombe huwawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo.*

# Halmashauri yaanzisha shamba darasa la miti Kata ya Mtwango.

Katika kutambua umuhimu wa kutoa elimu kwa njia ya vielelezo na kutunza mazingira Halmashauri ya wilaya ya Njombe, imeanzisha kitalu cha miche ya miti katika kijiji cha Lunguya kilichopo Kata ya Mtwango wilayani Njombe.

Hadi sasa jumla ya miche ya miti aina ya mikalatusi 16,920 tayari imependwa katika kitalu hicho na inasimamiwa na wataalamu kutoka katika Halmashauri.

Kuwepo kwa kitalu hiki kunaongeza wigo wa utoaji wa elimu ya ugani-misitu kwa vitendo katika maeneo ya Halmashauri ya wilaya pamoja na kuongeza kasi ya utunzaji wa mazingira.

Halmashauri imeanzisha kitalu hiki ikiwa ni moja ya mkakati wa uwekezaji ili kuiongezea mapato pamoja na kuongeza nguvu ya kuzisaidia taasisi za elimu kukabiliana na uhaba wa madawati na vikundi mbalimbali vyenye mahitaji maalum ya kuanzisha mashamba ya miti.

Msimu huu wa mvua Halmashauri itasambaza miche 1000 kwenye kila Kata kwa ajili ya kuigawa kwenye kila shule ili iweze kutumika kutengenezea madawati na meza hapo baadae pamoja na taasisi mbalimbali za Umma kwenye maeneo ya Kata.

Sambamba na hilo Halmashauri inatarajia kusambaza miche iliyooteshwa kwa vikundi vya kijamii ikiwemo yatima, vijana na wanawake ili kuongeza nguvu ya kipato kwa makundi mbalimbali na mingine itauzwa kwa ajili ya kuongeza mapato.

Katika kuhakikisha kuwa mpango huu unakuwa endelevu Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imeweka mikakati ya kupanua wigo wa uoteshaji wa miche ya miti kwa kuongeza ukubwa wa kitalu pamoja na kufanya mipango ya kuanzisha kitalu kingine katika Kata ya Matembwe.

Halmashauri inatarajia kupanua wigo wa aina ya miche inayooteshwa ikiwemo ile inayokuwa haraka pamoja na miti rafiki ya maji kwa ajili ya kupanda kwenye vyanzo vya maji,miche ya matunda, mapambo , kivuli na mazao mengine ya misitu.

Aidha, Halmashauri inatarajia kuanzisha shamba la miti lenye zaidi ya hekari 1000 katika kijiji cha nyave ikiwa ni sehemu ya uwekezaji wa Halmashauri katika sekta ya misitu.

Tangu kuanzishwa kwa kitalu hiki wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya Halmashauri wamekuwa wakijitokeza kwa nyakati tofauti kupata elimu ya uanzishaji wa kitalu cha miti, usimamizi na uendeshaji, elimu ambayo inatolea bure kwa wananchi wote.



*Madiwani na wataalaum wa halmashauri wakikagua kitalu cha kuotesha miche kilichoanzishwa na Halmashauri kijiji cha Lunguya Kata ya Mtwango ikiwa ni moja ya uwekezaji na shamba darasa .*



*Mkuu wa wilaya ya njome Bi Luth Msafiri akizungumza na wanawake waliofika zahanati ya Nyombo kuwaandikisha watoto wao katika kampeni ya kusajili watoto chini ya umri wa miaka mitano*



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe Monica PZ Kwiluhya akisoma taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe Christopher Ole Sendeka Njombe alipofanya ziara ya kujitambulisha katika Halmashauri.*



*Naibu waziri Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki Kikanda na Kimataifa (MB) Dr Suzan Kolimba (mwenye kitambaa kichwani) akikabidhi vitabu vya sayansi Shule ya Sekondari Ikuna.*



*Madiwani pamoja na wataalaumu wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe choo na miundombinu ya kunawa mikono katika shule ya msingi Matembwe wakati wa kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri robo ya pili ya mwaka.*



*Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe pamoja na wataalam wakikagua ujenzi wa kisima cha maji kwenye shule ya Msingi Isoliwaya katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.*



*Baadhi ya wananchi na wataalaum wa Halmashauri wakifanya usafi kutekeleza agizo la rais wa Jamhuri ya Muungano waTanzania John Pombe Magufuli ya kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi kufanya usafi. Hapa ni Kata ya Mtwango.*



*Kaimu Mkuu mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Michael Banyemaa akitoa mafunzo kwa madiwani wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe juu ya muundo wa kamati za afya ya msingi.*



*moja ya Mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule ya Sekondari Mulunga Iliyopo katika Kata ya Ukalawa Halmashauri ya wilaya ya Njombe ambao ujenzi wake umekamilika.*



*Naibu waziri wa ardhi nyumba na maendeleo ya makazi Angeliana Mabula (kushoto) akiwa na mkuu wa wilaya ya njombe Luth Msafiri (wakwanza kulia) wakati wa ziara ya naibu waziri kukagua mifumo ya ukusanyaji kodi za majengo katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.*



*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya wilaya ya Njombe Bi. Monica PZ Kwiluhya akiwaonyesha wakuu wa idara (hawapo pichani) tuzo ambazo halmashauri imepata kuhusu masuala ya fedha na Mipango.*





*Pichani kushoto na kulia ni wakuu wa Idara na vitengo wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe wakifuatila kwa mkini mjadala wabajeti ya Halmashauri kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 katika kikao cha baraza la madiwani kwa ajili ya kupitia rasimu ya bajeti ya Halmashauri*